

Maswali


1. Mbona Musa alienda Midiani?
2. Musa alioa nani?
3. Mbona Waisraeli hawakukuwa na furaha huko Misri?
4. Waisraeli waliuliza nani kuwasaidia?
5. Musa aliona kitu gani cha ajabu alipokuwa kwa mlima wa Herobu?
6. Nani alizungumza na Musa kutoka kwa kijiti kilichowaka?
7. Mungu aliambia Musa kwamba alimchagua kufanya nini?
8. Mungu aliahidi Musa nini?
9. Mungu aliambia Musa awapeleke Waisraeli wapi?
10. Mungu alituma nani kusaidia Musa?

Majibu

1. Farao alikasirikia Musa kwa hivyo Musa alitorokea Midiani.
2. Musa alioa Zipora.
3. Waisraeli hawakuwa na furaha kwa sababu Wamisri waliwateza.
4. Waisraeli waliuliza Mungu awasaidie.
5. Musa aliona kijiti kikiwaka kwa moto lakini hakikuchomeka.
6. Mungu alisema na Musa kutoka kwa kijiti kilichowaka.
7. Mungu alikuwa amemchagua Musa kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri.
8. Mungu aliahidi kusaidia Musa.
9. Mungu aliambia Musa awapeleke Waisraeli mpaka kwa nchi aliyoahidi Ibrahimu, Isaka na Yakobo.
10. Mungu alituma Haruni nduguye Musa ili amsaidie.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



13 Musa kwa kijiti kinachowaka

Marejeo

Kutoka 3:1 – 17 na 4: 1 – 17

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alimchagua Musa ili awatoe Waisraeli kutoka Misri. Mungu aliahidi kusaidia Musa.

Maneno maalum

- 13.1 Farao ana hasira + Musa alitoroka + Midiani + kisima + oa + kondoo
13. 2 Misri + Waisraeli + hana furaha + ombo + Mungu + Musa + kiongozi
13. 3 Musa + kondoo + jangwani + Herobu + kijiti + waka
- 13.4 Malaika + Musa + vua viatu + mahali patakatifu + Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo + Musa + kiongozi
- 13.5 Mungu + saidia + Musa + ongoza + Nchi ya Ahadi + Haruni + Misri + Farao + acha Waisraeli waende

13.1 Siku moja Farao alikasirikia Musa sana hata alitaka kumuua. Musa aliogopa na akatoroka. Musa alisafiri mwendo mrefu hati akafika kwa nchi ya Midiani. Alifika kwa kisima cha maji. Kulikuwa na wanawake walikuwa wakipea kondoo za baba yao maji. Musa aliwasaidia kupea kondoo wale maji.

Musa aliishi na familia moja kule Midiani. Alisaidia kuwachungia kondoo. Baadaye alioa bintiye mmoja aliyeitwa Zipora. Walipata wana wawili. Musa aliishi nao kwa muda ya mwaka mmoja na alikuwa akichunga kondoo. Wakati mwengine Musa alikuwa akipeleka kondoo mbali jangwani kuwatafutia nyasi na maji.

13.2 Huko nyuma yake kwa nchi ya Misri, Waisraeli walikuwa na huzuni. Walikuwa watumwa na Wamisri walikuwa wabaya sana kwao. Mambo yalipowaendea vibaya sana, walikumbuka vile Mungu alisaidia baba zao –Ibrahim, Isaka na Yakobo (jina lililo badilishwa kuwa Israeli).

Waisraeli waliomba Mungu wakimuuliza awasaidie. Kawaida Mungu husikia maombi ya watu wakimwomba. Kwa hivyo Mungu alisikia maombi ya Waisraeli. Mungu alifanya mpango wa kuwasaidia watoke Misri. Mungu alichagua Musa awe ndiye kiongozi wa kutoa Waisraeli Misri. Musa alikuwa mtu mzuri tena mjasiri. Alipenda Mungu na kumtii. Angekuwa kiongozi mzuri.

13.3 Siku moja Musa alipeleka kondoo mbali kule jangwani akiwatafutia nyasi na maji. Aliongoza kondoo mpaka juu ya mlima wa Herobu. Kwa umbali, Musa aliona kijiti kinawaka kwa moto. Alishangaa alipokuwa akiangalia hicho kijiti. Miali ya moto iliendelea kuwaka lakini kijiti hakikuungua. Musa alienda kuangalia kijiti kilichokuwa kikiwaka moto.

13.4 Moto ule wa kijiti kwa kweli alikuwa malaika aliywonekania Musa. Musa alipokuja karibu na kijiti, Mungu alimwita, "Musa! Musa!" Musa alijibu, "Mimi hapa." Mungu aliambia Musa, "Usikaribie hapo. Vua viatu vyako, kwa sababu mahali penye umesimama ni pahali patakatifu. Mimi ni Mungu wa Ibrahim, Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo."

Musa alivua viatu na akapiga magoti ili asikilize Mungu. Mungu aliambia Musa kwamba Waisraeli wanahuzuni kwa sababu ya utumwa. Wamisri walikuwa wanawadhulumu. Mungu aliambia Musa kwamba Waisraeli walikuwa wamemwomba awasaidie. Mungu alisema kwamba alikuwa amemchagua Musa kwenda kuwaokoa kutoka kwa Wamisri. Musa alikuwa na uoga. Hakutaka kurudi Misri. Hakutaka kuwaongoza Waisraeli watoke Misri.

13.5 Mungu aliahidi kwamba atamsaidia Musa. Mungu atamlinda Musa na kumsaidia awaongoze Waisraeli watoke Misri. Mungu aliahidi Musa kwamba atamsaidia awaongoze Waisraeli waende kwa nchi nzuri aliyoahidi Ibrahim, Isaka na Yakobo. Mungu alituma Haruni nduguye Musa ili amsaidie.

Musa alirudisha kondoo nyumbani. Halafu akachukuwa mkewe na wanawe na kurudi Misri. Mungu aliambia Musa na Haruni waende wamuulize Farao awaruhusu Waisraeli waondoke Misri na warudi kwa nchi yao.

